**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI**

# MAELEZO YA MHESHIMIWA PROF. KITILA ALEXANDER MKUMBO (MB.), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI, AKIWASILISHA MAPENDEKEZO YA SERIKALI YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2024/2025

**DODOMA**

**MACHI 11, 2024**

**MAELEZO YA MHESHIMIWA PROF. KITILA ALEXANDER MKUMBO (MB.), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI, AKIWASILISHA MAPENDEKEZO YA SERIKALI YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2024/2025**

**Dodoma, Jumatatu 11 Machi 2024**

---

## 1. SALAMU

*1.1* ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** awali ya yote, ninamshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, na hivyo kunipa heshima hii kubwa ya kusimama mbele ya Bunge lako na mbele ya waheshimiwa wabunge wenzangu kuwasilisha mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/2025.

*1.2* ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Tunapoelekea kuadhimisha miaka mitatu tangu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akabidhiwe uongozi wa nchi yetu, ninamshukuru Rais wetu kwa uongozi wake makini, imara na wenye maono ya mbali na ambao umeweka maslahi ya Taifa, kizazi cha leo na vizazi vijavyo mbele. Uongozi wake makini unaozingatia haki, utawala wa sheria na misingi ya demokrasia umeiwezesha nchi yetu kuwa na utulivu mkubwa wa kisiasa na hivyo kuendelea kudumisha amani, umoja na mshikamano ambazo ni tunu mama kwa nchi yetu. Aidha, kupitia uongozi wake na maono yake, nafasi na mchango wa nchi yetu katika jumuiya ya kimataifa unaonekana, unatambulika, na unaheshimika. Kwa kifupi, chini ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Chama Cha Mapinduzi, Taifa letu lipo salama kisiasa, kiuchumi, kijamii na katika nyanja zote za maendeleo.

*1.3* ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** ninawashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isidori Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu, kwa jinsi wanavyomisaidia Mheshimiwa Rais katika kuongoza nchi na kwa usimamizi wao makini wa utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais na Ilani ya CCM kwa ujumla. Ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, kwa kuendelea kuiongoza vyema

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Aidha, ninawashukuru Dkt. Tausi Kida, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Ndugu Lawrence Mafuru, Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, na watumishi wote wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Tume ya Mipango kwa ushirikiano walionipa katika kuandaa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25.

*1.4* ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Ninaungana na watanzania wote kumpa pole Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, familia na watanzania wote kutokana na misiba mikubwa ya kitaifa iliyotukumba hivi karibuni kufuatia kufariki kwa wapendwa wetu, Mheshimiwa Ally Hassan Mwinyi, Rais wa awamu ya pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowasa, aliyekuwa Waziri Mkuu mstaafu. Kwa kipekee kabisa ninawapa pole waheshimiwa wabunge wenzetu, Mheshimiwa Abdullah Ally Mwinyi, Mbunge wa Mahonda na Mheshimiwa Fredrick Edwad Lowassa, Mbunge wa Monduli, kwa kuondokewa na wazazi wao. Tunaendelea kuwaombea ili Mungu aendelee kuwapa nguvu katika kukabiliana na kipindi hiki kigumu. Tunawaombea viongozi wetu hawa waliotangulia mbele za haki pumziko la amani. Amina!

## 2. UTANGULIZI

*2.1* ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/2025 yanawasilishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 116 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023. Maelezo yangu nimeyaweka katika sehemu kuu tano, ambazo ni: Utangulizi; Tathmini ya Mwenendo wa Hali ya Uchumi; Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/2024; Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/2025; na Hitimisho.

*2.2* ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/2025 yamezingatia miongozo na mikakati ya maendeleo ya kitaifa, kikanda na kimataifa ikiwemo: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063; Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) 2050; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini

mwa Afrika (SADC) 2050; na matokeo ya tathmini ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

*2.3* ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Aidha, mapendekezo haya yamezingatia kikamilifu maoni na ushauri wa waheshimiwa wabunge waliyoyatoa wakati wa mjadala wa kujadili mwelekeo wa mpango wa maendeleo katika Mkutano wa 13 wa Bunge uliofanyika mwezi Novemba 2023. Kupitia maoni na ushauri wao, waheshimiwa wabunge waliainisha maeno kumi (10) ambayo ni muhimu mpango ujao wa maendeleo uyazingatie. Maeneo haya ni: *miundombinu, kilimo, mifugo na uvuvi, nishati, utalii, viwanda, biashara na uwekezaji, ushiriki wa sekta ya binafsi, uchumi wa gesi, utafiti na maendeleo (R&D), kutumia fursa zitokanazo na mabadiliko ya tabia nchi (kama vile uvunaji wa hewa ukaa),* na *kutumia fursa za kijiografia*. Aidha, waheshimiwa wabunge walisisitiza serikali kuja na mpango madhubutu wa kushughulikia changamoto za hifadhi na migogoro ya ardhi. Ninapenda kulihakikishia Bunge hili tukufu na waheshimiwa wabunge kuwa mapendekezo ya mpango ninayowasilisha leo, pamoja na mipango ya kisekta itakayowasilishwa katika mkutano ujao wa Bunge, yamezingatia maoni na ushauri wao kikamilifu.

## 3. MWENENDO WA HALI YA UCHUMI

*3.1* ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Tathmini ya mwenendo wa hali ya uchumi inaonesha kuwa uchumi wa Tanzania uliendelea kuhimili changamoto za kiuchumi za kidunia kama vile mabadiliko ya tabia nchi na vita nchini Ukraine na ukanda wa Gaza, na kubadilika kwa sera za fedha nchini Marekani, ikiwemo kupandisha riba katika fedha zinawekezwa ndani ya nchi yao. Pato la Taifa liliongezeka kutoka shilingi trilioni 124.2 katika kipindi cha Januari – Septemba 2022 hadi kufikia shilingi trilioni 140.0 katika kipindi cha mwezi Januari hadi Septemba 2023. Aidha, Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2015 liliongezeka hadi shilingi trilioni 109.2 katika kipindi cha mwezi Januari hadi Septemba 2023 kutoka shilingi trilioni 103.7. Uchumi wa Taifa ulikua kwa asilimia 5.3 katika kipindi cha Januari – Septemba 2023 ukilinganisha na asilimia 5.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2022.

*3.2* ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Ukuaji huo ulichangiwa na jitihada mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ya awamu ya sita ikiwemo: mikakati ya kukabiliana na athari za vita kati ya Ukraine na Urusi; uwekezaji wa kimkakati katika

miundombinu ya nishati, maji, afya, elimu, barabara, reli na viwanja vya ndege; kuongezeka kwa uzalishaji wa madini, hususan dhahabu na makaa ya mawe; na kuongezeka kwa mikopo katika sekta binafsi ambayo imechochea shughuli za kiuchumi.

*3.3* ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Sekta zilizokua kwa kasi kubwa katika kipindi cha marejeo ni pamoja na: Fedha na bima (asilimia 16.0); uchimbaji madini na mawe (asilimia 10.2); umeme (asilimia 10.0); huduma nyingine ikijumuisha sanaa na burudani (asilimia 10.0); malazi na chakula (asilimia 8.9); na habari na mawasiliano (asilimia 7.9). Aidha,Katika kipindi hicho Shughuli za uchumi zilizokuwa na mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa ni pamoja na kilimo (asilimia 24.8), ujenzi (asilimia 13.6), uchimbaji madini na mawe (asilimia 9.7), biashara na matengenezo (8.4), uchukuzi na uhifadhi wa mizigo (asilimia 7.2), na viwanda (asilimia 6.9).

*3.4* ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Katika kipindi cha mwezi Januari, 2024 mfumuko wa bei nchini ulifikia asilimia 3.0 ikilinganishwa na asilimia 4.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Aidha, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2022. Kiwango hiki kipo ndani ya malengo ya kati ya asilimia 3.0 hadi 7.0. Hali hii imetokana na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti na kuanza kuimarika kwa upatikanaji wa mazao ya chakula katika masoko ya ndani na ya nchi jirani.

## 4. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2023/24

*4.1* ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Serikali inatekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (The Third Five Year Development Plan - FYDP III 2021/22 – 2025/26), ikiwa ni moja ya nyenzo ya kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Dhima ya mpango huu ni “Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu”. Mpango huu una maeneo makuu matano ya kipaumbele, ambayo ni: *kuchochea uchumi shindani na shirikishi, kuimarisha uwezo wa uzalishaji na utoaji wa huduma, kukuza uwekezaji na biashara, kuchochea maendeleo ya watu,* na *kuendeleza raslimali watu*.

*4.2* ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Kwa ujumla wake, FYDP III una viashira na shabaha za

jumla 15 ambavyo vimegawanywa katika makundi matatu makubwa: kuchochea uchumi shindani, kuchochea maendeleo ya watu na ustawi wa jamii, na kuendeleza raslimali watu. Hapa chini, ninaeleza kwa muhtasari miradi na programu zilizotekelezwa katika mwaka 2023/2024, mafanikio yaliyopatikana na hatua iliyofikiwa katika kufikia shabaha zilizowekwa.

*4.3* ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Baadhi ya miradi na programu zilizotekelezwa katika ***kuchochea uchumi shindani*** ni kama ifuatavyo:

i) Serikali iliendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa (Standard Gauge Railway-SGR). Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu hadi kufikia Disemba 2023 ni kama ifuatavyo: kipande cha *Dar es Salaam – Morogoro* (km 300) utekelezaji umefikia asilimia 98.84 (pamoja na ujenzi wa njia ya kuelekea bandarini (asilimia 72.54); kipande cha *Morogoro – Makutupora* (km 422) umefikia asilimia 96.35; kipande cha *Mwanza - Isaka* (km 341) asilimia 52.69; *uundaji wa vichwa viwili (2) vya treni vya njia kuu aina ya 88U na vichwa saba (7) vya sogeza aina ya 64XX* umefikia asilimia 62; na kuendelea na ukarabati wa njia ya MGR ya Kaliua-Mpanda (Km 210) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 10.53.

ii) Serikali iliendelea na ujenzi **Daraja la Kigongo – Busisi (Mwanza);** pamoja na barabara unganishi zenye urefu wa km 1.66 ambapo ujenzi umefikia asilimia 80.1.

iii) Serikali iliendelea na utekelezaji wa **Mradi wa Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL)** ambapo katika kipindi hiki ndege moja (1) aina ya Boeing 737-9 Max ilipokelewa; kulipa sehemu ya malipo ya ndege aina ya Boeing 737 Max 9, Boeing 787-8 na Boeing 737-7.

iv) Serikali iliendelea kuboresha na kupanua mtandao wa barabara na madaraja nchini na zile zinazounganisha Tanzania na nchi jirani. Katika kipindi hiki, miradi ifuatayo ilikamilika: ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami km 115.97, barabara za changarawe km 3,080.87, madaraja makubwa 21, kalavati 17 na mifereji ya maji yenye urefu wa mita 51,309.62 na matengenezo ya barabara km 9,838.8.

v) Serikali iliendelea kuboresha bandari na shughuli zake ikiwemo: kuendelea na uchimbaji na upanuzi wa lango la kuingilia na kugeuzia meli hadi kufikia kina cha mita 15.5 katika Bandari ya Dar es salaam ambapo utekelezaji umefikia asilimia

99.9; kukamilika kwa uboreshaji wa Bandari ya Tanga unaohusisha kazi ya kuongeza kina kutoka kina cha maji cha mita tatu (3) hadi mita 13; kuimarisha na kuboresha Gati Na. 1 - 2 zenye urefu wa mita 450; na kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya zege yenye urefu wa kilomita 15.5 kutoka barabara kuu ya Morogoro hadi Vigwaza/Kwala. Aidha, Serikali ilikamilisha mchakato wa kupata mwekezaji wa kuwekeza, kuendeleza na kuendesha Bandari ya Dar es Salaam. Baada ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuridhia mkataba wa ushirikiano wa kiuchumi (IGA) kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mamlaka ya Falme ya Dubai mwezi Juni 2023, tarehe 22 Oktoba 2023 mikataba mitatu ya utekelezaji wa miradi katika kuwekeza na kuendesha Gati za 0-3 na Gati za 4-7 ilisainiwa kati ya TPA na Kampuni ya DP World. Kufuatia hatua hii, Serikali inatarajia kuwa mapinduzi makubwa ya kiuwekezaji, kiuendelezaji na kiutendaji yatatokea katika Bandari ya Dar es Salaam katika siku chache zijazo.

vi) Serikali iliendelea kutekeleza mradi wa **Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (MW 2,115)** ambapo kwa wastani utekelezaji wake umefikia asilimia 96.9. Kufuatia hatua hii, mwezi Februari 2024 majaribio ya kuzalisha umeme yalifanikiwa na tayari megawati 235 zimeshaanza kuzalishwa na kuingizwa kwenye gridi ya Taifa. Tunampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake thabiti katika kuhakikisha mradi huu unakamilika. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko na mawaziri waliomtangulia katika Wizara ya Nishati kwa usimamizi wao madhubuti wa mradi huu.

vii) Serikali iliendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kuimarisha teknolojia ya habari na mawasiliano. Hii ni pamoja na kufikisha huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwenye wilaya 21 (asilimia 91) kati ya wilaya 23; kuendelea na ujenzi wa mkongo wa Taifa wa mawasiliano kuunganisha Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kupitia ziwa Tanganyika; kuendelea na ujenzi wa kilometa 1,600 za Mkongo wa Taifa (asilimia 87); na kuendelea kuunganisha taasisi 50 (asilimia 25); na kuendelea na usajili wa anwani za makazi ambapo anwani 12,385,956 zimesajiliwa.

viii) Katika kuongeza tija ya uzalishaji katika kilimo, hatua zifuatazo zilichukuliwa:

a. Katika kuimarisha upatikanaji wa pembejeo kupitia mpango wa ruzuku kwa wakulima (ruzuku ya mbegu, mbolea, viuatilifu na zana za kilimo), tani 58,807.61 za mbegu bora zilisambazwa kwa wakulima na tani 797,871 za mbolea zilisambazwa, zikiwemo tani 418,942 zilizouzwa kwa wakulima 3,751,688 kwa bei ya ruzuku katika mikoa 26

b. Katika kukuza na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji, serikali iliendelea na ujenzi wa skimu 22 za umwagiliaji ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 76 na ukarabati wa skimu 21 ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 70 na ujenzi wa mabwawa 11 ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 70.

c. Katika kuimarisha usalama wa chakula, serikali iliendelea na ujenzi wa maghala 28 yenye uwezo wa kuhifadhi tani 33,000 katika Mkoa wa Ruvuma ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 75, na ujenzi wa maghala na vihenge katika kanda saba za NFRA zenye uwezo wa kuhifadhi tani 501,000 ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 85

i) Serikali iliendelea na utekelezaji wa programu ya Jenga Kesho Iliyobora (***Building Better Tomorrow -BBT****)* yenye kulenga kubadilisha kuzalisha ajira kwa vijana na wanawake kupitia kilimo biashara. Lengo la programu hii ni kuongeza ushiriki wa vijana na wanawake katika kilimo kwa kuwapatia mafunzo ya kilimo biashara na kuwahakikishia upatikanaji wa ardhi, mitaji na masoko. Katika kutekeleza programu hii, mashamba makubwa yenye ukubwa wa ekari 999,706.6 katika mikoa kumi yamebainishwa na mashamba matatu yenye ukuwa wa ekari 64,552 yanaendelezwa. Vijana 268 walipatiwa mafunzo ya kilimo biashara na kupatiwa mashamba yenye ukubwa wa ekari 365.8 ambazo zimepandwa zao la alizeti.

ix) Katika kuimarisha afya ya mifugo na kuongeza thamani mazao ya mifugo na uvuvi, serikali iliendelea na ujenzi wa maabara ya virusi ili kuzalisha aina 13 za chanjo dhidi ya magonjwa ya kipaumbele ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 20; mifugo 24,114,334 ilichanjwa dhidi ya magonjwa mbalimbali, na ng'ombe 2,300 walinenepeswa kupitia vituo nane vya utafiti wa mifugo. Aidha, serikali ilianza ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ya Kilwa (mkoani Lindi) ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia nane.

x) Katika kuimarisha na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini, na kama sehemu ya utekelezaji Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara

(MKUMBI), hatua zifuatazo zilitekelezwa:

a. Sheria ya uwekezaji ilihusishwa na kuandikwa upya
b. Tozo, ada na faini 106 katika sekta za biashara na uwekezaji zilifutwa au kurekebishwa
c. Kujenga mfumo wa pamoja wa huduma kwa wawekezaji nchini (Tanzania Electronic Investors' Window – TeIW) ambapo taasisi za umma saba zinazohudumia wawekezaji zimeunganishwa
d. Kufanyika kwa makongamano kumi ya biashara na uwekezaji
e. Kusainiwa kwa hati kumi za kuvutiia uwekezaji kati ya Tanzania na nchi mbalimbali
f. Kuzinduliwa kwa mfumo wa taarifa za masoko uitwao TanTrade Biashara Mobile App ambao unawawezesha wafanyabishara kupata taarifa za masoko ya bidhaa zinazozalishwa nchini.

*4.4* ***Mheshimiwa Mwenyekiti****,* Kutokana na utekelezaji wa miradi na programu zilizotajwa hapo juu katika kuchochea uchumi shindani, matokeo na mafanikio yafuatayo yamepatikana.

ii) Ujenzi wa reli ya SGR kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro upo katika hatua za mwisho na sasa upo katika hatua ya majaribio.

iii) Kufuatia kujaa kwa maji katika Bwawa la Julius Nyerere, kiwango cha kuzalisha umeme kimeongezeka kutoka megawati 1,676.35 na kufikia megawati 1,911.35, ikilinganishwa na lengo la kufikia megawati 4,915 ifikapo mwaka 2025. Hali hii imeifanya nchi iweze kujitosheleza katika uzalishaji wa umeme na kuondoa hali ya mgao wa umeme uliokuwepo, aghalabu kwa sasa.

iv) Kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya mbegu bora, kuongezeka kwa matumizi ya mbolea na kuongezeka kwa eneo la umwagiliaji kutoka hekta 300,000 mwaka 2019/2020 hadi kufikia hekta 800,000 mwaka 2023, kiwango cha uzalishaji kimeongezeka na hali ya usalama wa chakula imeimarika. Uzalishaji wa mazao ya chakula umeongezeka kutoka tani 17,148,290 mwaka 2021/2022 hadi kufikia tani 20,402,014 mwaka 2022/2023, ikiwa ni ongezeko la asilimia 19 katika kipindi cha mwaka mmoja. Hali hii imeimarisha hali ya usalama wa chakula nchini ambapo hali ya utoshelevu wa chakula imefikia asilimia 124 mwaka 2022/2023

ikilinganishwa na lengo la kufikia asilimia 130 ifikapo mwaka 2025/2026.

v) kuongezeka kwa idadi ya watalii wa kimataifa kutoka watalii 1,454,920 mwaka 2022 hadi kufikia watalii 1,808,205 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asimilia 24.28. Hii imesababisha kuongezeka kwa mapato ya utalii kutoka dola za Marekani milioni 2,527.77 mwaka 2022 hadi kufikia dola za Marekani milioni 3,373.83 mwaka 2023, ukilinganisha na lengo la kufikia dola za kimarekani milioni 6,000 ifikapo mwaka 2025.

vi) Kutokana na kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini, idadi ya miradi inayosajiliwa katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania (Tanzania Investment Centre – TIC) imeongezeka kutoka miradi 293 iliyosajiliwa mwaka 2022 hadi kufikia miradi 526 iliyosajiliwa mwaka 2023. Idadi ya ajira zinazotokana na miradi ya uwekezaji iliongezeka kutoka 40,889 mwaka 2022 hadi ajira 137,010 mwaka 2023. Aidha, kiwango cha mtaji kutokana na miradi kiliongezeka kutoka dola za kimarekani milioni 4,537.10 mwaka 2022 hadi kufikia dola za kimarekani milioni 5,720, ukilinganisha na lengo la kuvutia mtaji wa dola za kimarekani milioni 7,980.7 ifikapo mwaka 2025.

vii) Katika kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani, kiwango cha mauzo ya bidhaa za viwandani (manufacturing goods) kiliongezeka kwa asilimia 20.8, kutoka dola za kimarekani milioni 1,340.5 mwaka 2022 na kufikia dola za kimarekani milioni 1,401.2 mwaka 2023.

*4.5* ***Mheshimiwa Mwenyekiti**,* Baadhi ya miradi na programu zilizotekelezwa katika ***kuchochea maendeleo ya watu na ustawi wa jamii*** ni kama ifuatavyo:

i) Ujenzi, upanuzi na uboreshaji wa miundombinu na vifaa tiba katika hospitali za kitaifa, kikanda, mikoa, wilaya, vituo vya afya na zahanati, ikiwemo:
   a. ujenzi wa hospitali 44 mpya katika ngazi ya halmashauri
   b. ujenzi wa maboma ya zahanati 378 katika Halmashauri 184
   c. uimarishaji wa huduma za chanjo ambapo jumla ya chanjo kwa watoto 1,507,919 zimetolewa
   d. ukarabati wa hospitali kongwe 31 za halmashauri ambapo utekelezaji umefikia asilimia 84.

ii) Kutungwa kwa sheria ya bima ya afya kwa wote

iii) Ujenzi, upanuzi na uboreshaji wa miundombinu ya kujifunza na kujifunzia katika ngazi zote za elimu, ikiwemo:

a. Kukamilika kwa ujenzi wa shule za msingi mpya 300
b. Kukamilika kwa ujenzi wa shule za sekondari 43 za sekondari za upili (A'level)
c. Kuendelea na ujenzi wa vyuo vipya vitatu vya ualimu
d. Kuchapa na kusambaza vitabu vya kiada 4,000,000 kwa ajili ya wanafunzi wa Darasa la I na II
e. Kuendelea na ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi 98
f. Kuendelea na utekelezaji wa programu ya kutoa elimu ya msingi na sekondari bila malipo
g. Kutolewa kwa mikopo kwa wanafunzi 222,131 wa alimu ya juu na wanafunzi 1,429 wa vyuo vya kati (stashahada)
h. Kufadhili wanafunzi 1,276 kupitia programu ya ufadhili ya Samia (*Samia Scholarship*)
i. Kuendelea na ujenzi wa majengo mapya 25 katika vyuo vikuu kupitia mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (Higher Education for Economic Transformation Project – HEET) ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 18
j. Kufadhili wahadhiri na watumishi 369 kuhudhuria mafunzo katika ngazi ya uzamili na uzamivu kutoka vyuo vikuu vya umma na binafsi
k. Kukamilika kwa mapitio ya sera na mitaala mipya ya elimu

iv) Kuendelea na utekelezaji wa miradi 1,546 ya usambazaji maji safi vijijini ambapo miradi 374 yenye vituo vya kuchotea maji 5,529 katika vijiji 884 imekamilika na inatoa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi 2,274,193

v) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya usambazaji maji safi na salama na usafi wa mazingira katika miji mikuu ya mikoa, wilaya na miji midogo

vi) Kuendelea na programu za kulinda na kuendeleza raslimali za maji nchini ambapo vituo vipya 15 vya kufuatilia raslimali za maji vimejengwa na vingine 161 kukarabatiwa. Aidha, ujenzi wa Kituo Mahiri cha Raslimali za Maji (Water Resources Centre of Excellence) Mjini Dodoma unaendelea ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 87.

*4.6* ***Mheshimiwa Mwenyekiti**,* Kutokana na utekelezaji wa miradi na programu zilizotajwa hapo juu katika ***kuchochea maendeleo ya watu (ustawi wa jamii)*** matokeo na mafanikio yafuatayo yamepatikana:

i) Kuendelea kuongezeka kiwango cha uandikishwaji cha watoto katika elimu ya msingi ambapo sasa kimefikia 108.5%

ii) Kuendelea kuongezeka kiwango cha uandikishwaji cha watoto katika elimu ya sekondari ambapo sasa kimefikia 48.2%

iii) Kuendelea kuongezeka kwa kiwango cha wanafunzi wanaoendelea na elimu ya sekondari hadi kufikia 70%

iv) Kupungua kwa idadi ya vifo vya akina mama wajawazito wakati wa kujifungua ambapo sasa ni vifo 104 katika kila akina mama 100,000 wanaojifungua

v) Kupungua kwa idadi ya vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano ambapo sasa ni vifo 43 katika kila watoto 1000 wanaozaliwa

vi) Kuendelea kuimarika kwa hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama ambapo hadi Desemba 2023 umefikia wastani wa asilimia 79.6 vijijini na asilimia 88 mijini.

vii) Hali ya rasilimali za maji nchini imeendelea kuimarika na bado inaridhisha. Hadi sasa, rasilimali za maji ambazo zinaweza kupatikana kwa mwaka (annual renewable water resources) ni mita za ujazo bilioni 126 ambazo ni sawa na wastani wa mita za ujazo 2,105.Takwimu hizi zinadhihirisha kuwa, Taifa liko juu ya wastani wa tafsiri ya uhaba wa maji unaokubalika kimataifa ambazo ni mita za ujazo 1,700 kwa mtu kwa mwaka (agreed watwer stress indicator). Aidha, Taifa letu limethibitisha uhimilivu mkubwa katika athari za madiliko ya tabianchi kupitia rasilimali za maji. Kwa mfano, usanifu wa bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere ulionesha kuwa katika hali ya kawaida, bwawa hilo lingejaa maji katika misimu miwili ya mvua, yaani miaka miwili. Hata hivyo, hadi Machi 2024 bwawa hilo limejaa maji kiasi cha mita za ujazo bilioni 32 kabla ya miaka miwili haijakamilika ambayo ni matokeo ya uhifadhi wa vyanzo vya maji pamoja na usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini.

## 5. MAPENDEKEZO YA YA MPANGO WA MAENDELEO YA TAIFA WA MWAKA 2024/25

***5.1 Mheshimiwa Mwenyekiti,*** lengo la Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25 ni ***kuendelea kuchochea kasi ya ukuaji uchumi ambao ni jumuishi, unaopunguza umaskini na kuleta ustawi kwa wote, unaozalisha ajira kwa wingi, na unaochochea mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani nje ya nchi***. Katika kufikia shabaha hii, msukumo utawekwa katika kuongeza tija ya uzalishaji na uongezaji wa thamani wa mazao katika sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi, misitu na madini; kuchochea na kuboresha ubora wa elimu na mafunzo katika ngazi zote; kuongeza na kuimarisha matumizi zaidi ya teknolojia, hususan teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA); kuongeza uzalishaji viwandani; na kuimarisha huduma bora za jamii kwa wote, ikiwemo huduma za afya na upatikanaji wa maji safi na salama kwa wote.

***5.2 Mheshimiwa Mwenyekiti***, kipaumbele kitawekwa katika kukamilisha programu na miradi ya maendeleo inayoendelea, hususan miradi ambayo ipo katika hatua za mwisho za ukamilishaji kama ilivyoainishwa katika maeneo makuu matano ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26). Miradi mipya itakayotekelezwa katika mwaka 2024/25 ni ile ambayo itaongeza kasi ya ukuaji wa uchumi, kutoa matokeo ya muda mfupi, kupunguza umaskini na kuongeza mapato ya Serikali hususan fedha za kigeni.

***5.3 Mheshimiwa Mwenyekiti***, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, pamoja na mambo mengine, umeainisha miradi 17 ya kielelezo ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kwa kuzingatia maoni na ushauri wa waheshimiwa wabunge waliotoa katika Bunge la 13 la Novemba 2023, Serikali itachambua miradi hii na kuona miradi ambayo inaweza kutekelezwa na kukamilishwa katika muda wa mpango uliobaki kwa lengo la kubaki na miradi itakayoharakisha kufikiwa kwa malengo na viashiria vya mafanikio vya mpango. Aidha, katika kipindi hiki, Serikali itaendelea kuratibu na kusimamia mchakato wa maandalizi ya Dira (mpya) ya Taifa ya Maendeleo 2050.

***5.4*** **Mheshimiwa Mwenyekiti,** Malengo na shabaha za uchumi jumla ni kama ifuatavyo:

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 5.4 mwaka 2024 kutoka matarajio ya ukuaji wa asilimia 5.2 mwaka 2023;

(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 7.0 katika muda wa kati;

(iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 15.7 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 15.3 mwaka 2023/24;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 12.8 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 kutoka matarajio ya asilimia 12.5 mwaka 2023/24;

(v) Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa asilimia 2.9 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 kutoka matarajio ya asilimia 2.8 ya mwaka 2023/24; na

(vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

***5.5 Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Misingi kumi itakazingatiwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25 kama ifuatavyo:

i) Kuendelea kuwepo kwa amani, usalama na utulivu wa ndani ya nchi, katika nchi jirani na duniani kwa ujumla
ii) kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa
iii) Kuendelea kudumisha utawala bora na utawala wa sheria nchini
iv) Kuendelea kuimarika kwa utoshelevu wa chakula nchini
v) Kuendelea kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za uwekezaji na biashara.
vi) Kuendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na majanga ya asili na yasiyo ya asili (ukame, vita, magonjwa ya mlipuko na mafuriko)
vii) Kuwa na raslimali watu wa kutosha na bora inayokidhi matakwa ya wakati ambayo yanatawaliwa na teknolojia na ubunifu
viii) Nidhamu katika matumizi ya fedha za umma
ix) Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, hususani kwa wafanyabiashara na wawekezaji wadogo na wakati wa ndani
x) Kuwa na nidhamu ya utekelezaji wa mambo tuliyopanga.

**5.6** ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, katika kuchochea ushindani wa kiuchumi na ukuaji wa uchumi jumuishi, jumla ya programu na miradi 100 itatekelezwa kama ilivyoanishwa katika Sehemu ya tatu ya kitabu cha mpango. Miradi hii ni pamoja na:

i) Kuendelea kutekeleza miradi ya kielelezo, ikiwemo mradi wa reli ya kisasa ya SGR na miradi ya kufua nishati ya umeme kama vile bwawa la kufua umeme la Julius Nyerere, Ruhudji, Rusumo, Rumakali, Kinyerezi, na miradi ya umeme wa jua na upepo.

ii) Kuendelea kupanua na kuimarisha miundombinu ya usafiri wa barabara, reli, anga, na majini, na utunzaji endelevu wa mazingira

iii) Kuhakikisha kuwa nchi inaimarisha matumizi ya gesi (CNG) katika uendeshaji wa magari ili kuanza kupunguza utegemezi wa mafuta ya kuagiza nje ya nchi

iv) Katika kuendelea kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya kilimo, kuongeza thamani mazao, kukuza na kuimarisha uwezo wa kutunza mazao katika kuimarisha usalama wa chakula na kukuza masoko ya mazao ya wakulima, Serikali itachukua hatua zifuatazo:

a. Kuendelea kufanya utafiti na kuzalisha mbegu bora hususani kwa mazao ya kimkakati.
b. Kuendelea kuimarisha huduma za ugani
c. Kuendelea kuimarisha na kupanua kilimo cha umwagiliaji, ikiwemo kukamilisha skimu 25, kukarabati skimu 30 na kukamilisha ujenzi wa mabwawa 14 ya kuvuna maji ya mvua
d. Kuimarisha upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima, ikiwemo kununua magari matano (5) yenye uwezo wa kubeba tani 30 za mbegu, kujenga maabara mbili za mbegu, kununua vifaa vya utafiti na kujenga maghala matatu ya kuhifadhia mbegu
e. Kuendelea kutekeleza programu ya BBT kwa kutambua na kuanisha mashamba mapya 30 katika mikoa mitano, kupima ardhi ya kilimo kwa ajili ya uwekezaji katika mikoa kumi, kutoa mafunzo kwa walengwa 1000, kutoa mikopo ya riba nafuu kwa vijana na wanawake na kuhamasisha uanzishwaji wa kampuni za ugani kwa kushirikisha vijana wanaohitimu mafunzo ya kilimo. Kuweka mazingira maalum katika kuvutia ujenzi wa viwanda vidogo vijijini kwa lengo la kufanya ongezeko la awali la thamani (primary processing) katika sekta za kimkakati, zikiwemo kilimo, mifugo, uvuvi, na misitu. Serikali itatumia sera za kifedha na kikodi ili kuvutia wawekezaji katika maeneo ya vijijini ili mazao ya kilimo, mifugo,

uvuvi na misitu yatoke vijijini yakiwa yameanza kufanyiwa uchakataji wa awali (*semi-processed)*. Viwanda vya vijijini vitabakisha thamani kubwa kijijini na kutoa nafasi ya ajira kwa vijana na wanawake ambao wengi wao sasa wana elimu ya sekondari.

v) Kuendelea kuhamasisha, kutangaza na kuwezesha uwekezaji, kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi

vi) Kupitia upya mfumo wa kodi ili kuweka mazingira ya kukua kwa wigo wa walipa kodi sambamba na ukuaji wa pato la taifa

vii) Kufanya tathmini ya mahitaji ya raslimali watu

viii) Kwa kuzingatia umuhimu wa dijitali (digitalisation) katika kuleta mapinduzi ya uchumi vijijini, Serikali itaanzisha mradi wa kujenga mfumo wa dijitali vijijini (rural broad band) ili kuwaunganisha wananchi vijijini katika uchumi wa taifa na kuongeza matumizi ya TEHAMA katika shughuli za kiuchumi na kijamii.

ix) Kwa kuzingatia nafasi ya madini katika kuendelea kukuza ujazo wa mauzo ya nje, na kwa kuzingatia umuhimu wa madini ya kimkakati (*critical raw materials*) katika kutimiza azima ya dunia ya kuzalisha nishati safi na salama kwa mazingira, tutaweka mazingira mahususi kwa lengo la kuvutia wawekezaji watakaokuwa tayari kujenga viwanda vya kuongeza thamani ya madini hapa nchini, hususani katika ujenzi wa viwanda vya kuzalisha betri za magari na mitambo.

***5.7 Mheshimiwa Mwenyekiti***, katika kuchochea maendeleo ya watu na ustawi wa jamii, jumla ya programu na miradi 62 itatekelezwa ikiwemo ifuatayo:

i) Kuendelea na upanuzi na uboreshaji wa miundombinu ya kutolea huduma za afya, pamoja na upatikanaji wa vifaa tiba

ii) Pamoja na hatua kubwa tuliyopiga kama nchi katika kutokomeza ugonjwa wa malaria ambapo maambukizo yamepungua kwa 55% na wagonjwa wanaolazwa kwa ugonjwa wa malaria kupungua kwa asilimia 61 tangu 2015, bado ugonjwa huu unaendelea tishio kwa afya za wananchi na kuwa ni miongoni mwa magonjwa yanaongoza katika kuua. Aidha, kiwango cha maambukizo bado kipo juu ikiwa ni asilimia 8.1. Ili kufikia lengo la kupunguza maambukizi ya vimelea vya ugonjwa wa malaria kufika asilimia 3.5 ifikapo mwaka 2025, Serikali itaelekeza nguvu katika programu za kuangamiza mazalia ya mbu kwa kutumia viuatilifu.

iii) Kuendelea kutekeleza miradi ya usambazaji maji na usafi wa mazingira, ikiwemo kuendelea na maandalizi ya kutekeleza mradi wa kusafirisha maji kutoka Ziwa

Victoria kwenda Singida na Dodoma kwa ajili ya maji safi ya kunywa na umwagiliaji

iv) Kuendelea na upanuzi na uboreshaji wa miundombinu ya kujifunza na kujifunzia, pamoja na upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika ngazi zote za elimu

v) Kuendelea na utekelezaji wa programu ya kutoa elimu ya msingi na sekondari bila ada

vi) Kutoa mikopo kwa wanafunzi 93,500 wa elimu ya juu na elimu ya kati, wakiwemo wanafunzi 10,000 wa mafunzo ya stashahada

vii) Kutekeleza sera na mitaala mipya ya elimu, ikiwemo mafunzo kwa walimu

## 6. HITIMISHO

**6.1** **Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika mapendekezo niliyowasilisha Serikali imeanisha kazi zilizofanyika na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa taifa wa mwaka 2023/2024, pamoja na malengo, shabaha na miradi ya kipaumbele katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa 2024/2025. Kwa ujumla wake, programu na miradi 212 ya maendeleo imetekelezwa kwa kuzingatia vipaumbele vitano vilivyopo katika mpango wa miaka mitano na sekta 12 zimehusika katika utekelezaji huo. Katika mapendekezo niliyowasilisha, Serikali imeweka kipaumbele katika kukamilisha miradi ya kielelezo pamoja na programu na miradi ya maendeleo inayoendelea, hususan iliyo katika hatua za mwisho za ukamilishaji. Lengo ni kuwianisha uhalisia wa mapato na matumizi ya Serikali ili kufikia matokeo tarajiwa ya utekelezaji wa miradi katika kipindi cha ukamilishaji wa Dira 2025 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26).

**6.2** ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Katika kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana katika utekelezaji wa miradi, Serikali imeimarisha mfumo wa tathmini na ufuatiliaji ambapo sasa katika kila wizara ya kisekta na taasisi za serikali zinazojitegema kuna idara inayohusika na tathmini na ufuatiliaji (M & E). Aidha, katika kuhakikisha usimamizi thabiti na ufanisi katika utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo, tutaendelea kuhamasisha watekelezaji wa miradi kutumia Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo (National Project Management Information System- NPMIS) ili kuhakikisha taarifa za miradi na programu zinapatikana kwa wakati ,hususan wakati wa ufuatiliaji na tathmini.

**6.3** **Mheshimiwa Mwenyekiti**, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/2025 utaenda sambamba na mchakato wa kuandika dira mpya ya maendeleo ya Taifa letu kufuatia kukamilika kwa Dira ya sasa ifikapo mwakani. Ninaomba kutumia nafasi hii kutoa wito maalum kwa wananchi wote kushiriki kikamilifu katika kutoa maoni yao kuhusu mwelekeo wa nchi yetu katika miaka 25 (au zaidi) ijayo. Aidha, serikali imeweka utaratibu maalum na wa uhakika kwa waheshimiwa wabunge, pamoja na makundi mbalimbali ya kijamii kutoa maoni yao kuhusu dira ijayo yan taifa ya maendeleo.

**6.4** ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, kama nilivyoainisha katika maelezo yangu, mafanikio mengi yamepatikana katika utekelezaji wa mpango wa mwaka huu. Nichukue nafasi hii kukishukuru sana Chama Cha Mapinduzi kwa sera zake makini zilizozaa Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, ambayo ndiyo msingi wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26. Ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake makini na thabiti katika kuhakikisha kuwa Ilani ya CCM inatekelezwa kikamilifu. Aidha, kwa ya niaba mawaziri wenzangu, ninamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa ubunifu, bidii na diplomasia kubwa katika kutafuta raslimali fedha na watu kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wetu wa maendeleo. Kwa kifupi, kama nilivyosema awali, chini ya uongozi makini wa CCM na usimamizi madhubuti wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, nchi yetu na taifa letu lipo mikononi salama kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na katika nyanja zote!

***Mungu Ibariki Tanzania; Mungu Ibariki Afrika!***

***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** baada ya maelezo hayo, ninaomba kuwasilisha.

Ahsanteni Sana kwa kunisikiliza.



Prof. Kitila Alexander Mkumbo (Mb)

**Waziri wa Nchi**

**Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji**

*Dodoma, Jumatatu 11 Machi 2024.*